Jichunguzeni Wenyewe (Examine Yourselves)

na

Ellis P. Forsman

Jichunguzeni Wenyewe

na

Ellis P. Forsman

Octoba 11, 2011.

Jichunguzeni Wenyewe

2 Kor. 13:5

Kama Yeremia alivyoulilia maangamizi ya mji ya Yerusalemu, aliwaita watu wajichunguse wenyewe na hivyo wamrudie Bwana.

Omb. 3:40-41, "*Na tuchunguze njia zetu na kuzijaribu, na kumrudia BWANA tena. Na tumwinulie Mungu aliye mbinguni mioyo yetu na mikono.*"

Akifundisha katika kushiriki meza ya Bwana kikamilifu, Paulo aliandika kwamba kunapaswa kuwa na wakati wa mtu kujichunguza ili kuona kama mtu yuko sahihi kushiriki mwili na damu ya Bwana.

1 Kor. 11:27-31, "*Basi kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana. Lakini mtu ajihoji mwenyewe na hivyo aule mkate na kukinywea kikombe. Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake kwa kutokuupambanua ule mwili. Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu, na watu kadha wa kadha wamelala. Lakini kama tungejipambanua nafsi zetu, tusingehukumiwa.*"

Baadae Paulo aliwatia changamoto Wakorintho: 2 Kor. 13:5, "*Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu? Isipokuwa mmekataliwa.*"

Katika kufanya hivyo, anatumia sentensi ya wakati uliopo "*chunguza*" na "*thibitisha*"; ikionyesha kujichunguza huko kulipaswa kuwa ni tendo endelevu!

Kiuhalisia hii inaleta maswali muhimu…

Kwa nini tujichunguze wenyewe?

Kwa kiwango gani tunapaswa kujichunguzaa wenyewe?

Ni maswali yapi tutakuwa tunajiuliza?

Katika somo hili, tungependa tuelekeze mitazamo yetu katika wito huu "Jichunguzeni wenyewe". Tunapofanya hivyo, ebu tujibu maswali ambayo tayari yameulizwa, tukianziaa na…

Kwa nini tunapaswa kujichunguza wenyewe?

Kuona kama tupo ndani ya imani.

Paulo alisema katika 2 Kor. 13:5, "*Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu? Isipokuwa mmekataliwa.*"

Neno "katika imani" inamanishaa kuwa Mkristo mwaminifu. Hivyo, tunapaswa kuchunguza kama ni waaminifu kwa Bwana au siyo! Tunapaswa kukumbuka kwamba hata ya kuanguka kupo.

Inawezekana tukaanguka kama tukiacha wokovu wetu. Heb. 2:1-4, "*Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyossikiwa tusije tukayakosa. Kwa maana ikiwa lile neno lililonenwa na malaika lilikuwa imara na kila kosa na uasi ulipata ujira wa haki, sisi je tutapataje kupona tusipojali wokovu mkuu namna hii? Ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale waliosikia; Mungu naye akishuhudu pamoja nao kwa ishara na ajabu na nguvu za namna nyingi, na kwa magawanyo ya Roho Mtakatifu, kama alivyopenda mwenyewe.*"

Inawezekana kuwa na moyo mwovu wa kutoamini. Heb. 3:12-14, "*Angalieni ndugu zangu, usiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai. Lakini mwonyane kila siku maadamu iitwapo leo ili mmoja wenu asifanywe mgumu kwa udanganyifu wa dhambi. Kwa maana tumekuwa washirika wa Kristo kama tukishikamana na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho;*"

Andiko hili linamanisha, hataivyo, ni kwamba ni rahisi KUJUA msimamo wa mtu mbele za Mungu. Hakika, Biblia iliandikwa kwa kusudi hili ili kwamba tujue.

- 1 Yohana 5:13, "*Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu.*"

- 1 Yohana 2:3, "*Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye ikiwa tunashika amri zake.*"
- 1 Yohana 3:14, "*Sisi tunajua ya kuwa tumepita toka mautini kuingia uzimani, kwa maana twawapenda ndugu. Yeye asiyependa, akaa katika mauti.*"
- 1 Yohana 3:24, "*Naye azishikaye amri zake hukaa ndani yake yeye naye ndani yake. Na katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa huyo Roho aliyetupa.*"

Kuangali kama Yesu Kristo yuko ndani yetu.

Paulo aliwapa changamoto Wakorintho kuzingatia kama Yesu Kristo alikuwa ndani yao. Kwamba Kristo anakaa ndani ya Mkristo ni mawazo mazuri.

Iliahidiwa na Yesu mwenyewe. Yohana 14:21-23, "*Yeye aliye na amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye, naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake. Yuda Isakariote akamwambia Bwana imekuwaje ya kwamba wataka kujidhihirisha kwetu wala si kwa ulimwengu? Yesu akajibu akamwambia mtu akinipenda, atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake na kufanya makao kwake.*"

Inaanzia pale tunapomvaa Kristo katika ubatizo. Gal. 3:26-27, "*Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.*"

Wakati fulani tunaweza kushangaa "jinsi" anavyokaa ndani yetu, lakini funguo hapa ni…

- Kujua kwamba anafanya!
- Kutambua kwamba kuna njia tunazoweza KUJUA kwamba anakaa! Na ndio maana inahitajika tujichunguze kila wakati!

Kuangalia kama tuna "*kukataliwa*" (kuachwa).

2 Kor. 13:5, "*Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe, kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu? Isipokuwa mmekataliwa."*

Inaeleweka kwamba Kristo yuko ndani ya Wakristo, isipokuwa "wamekataliwa "*kukataliwa*" kunamanisha nini?

Hapa kuna baadhi ya nakala za Biblia inasema…

- "*mmekataliwa*" (KJV, ASV).
- "*Umeshindwa mtihani*" (NASV, NIV)
- "*isipokuwa hakika hamna sifa*" (NKJV)

Kiuhalisia, "*kutovumilia majaribu*", na katika mazingira ya kifungu inaongelea jaribio la…

- Kuwa katika imani
- Kuwa na Kristo ndani yenu.

Kifungu hiki ni miongoni mwa vifungu vinavyofunua kwamba Mkristo anaweza kuanguka kutoka katika imani!

Paulo alionya kuhusu kuanguka kutoka katika imani. Gal. 5:4, "*Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria.*"

Petro vilvile alionya kuhusu kuanguka kutoka katika kusimama imara. 2 Pet. 3:17, "*Basi mkitangulia kujua hayo, jilindeni nafsi zenu msije mkachukuliwa na kosa la hao wahalifu mkaanguka na kuuacha uthibitifu wenu.*"

Yesu aliongelea ambacho kingetokea kwa yale matawi ambayo hayakuzaa matunda.

- Yohana 15:1-2, "*Mimi ndimi mzabibu wa kweli na Baba yangu ndiye mkulima. Kila tawi ndani yangu lisilozaa huliondoa; na kila tawi lizaalo hulisafisha ili lizidi kuzaa.*"
- Yohana 15:6, "*Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea.*"

Kupitia uchunguzi binafsi mtu anaweza KUJUA mazingira ya hali halisi ilivyo!

Kujua kama tunajitambua wenyewe.

Kama Paulo anavyoita uchunguzi binafsi, anauliza "*Au hamjijui wenyewe?*"

Tunaweza kuangukia mtego kirahisi katika udanganyifu. Yakobo 1:22-25, "*Lakini iweni watendaji wa neno wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu. Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo. Maana hujiangalia, kisha huenda zake mara akasahau jinsi alivyo. Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake.*"

Dini mtu huyo ni "hasara" (haifai). Yakobo 1:26, "*Mtu akidhani ya kuwa anayo dini, wala hauzuii ulimi wake kwa hatamu hali akijidanganya moyo wake, dini yake mtu huyo haifai.*"

Ni katika uchunguzi binafsi wa kila mara tunaweza kujidanganya wenyewe! Hitaji halijawahi kuwepo katika "*kujichunguza wenyewe*", katika "*kujithibitisha wenyewe*". Hii inaongoza katika swali linalofuata…

Kwa viwango gani tunapaswa kujichunguza wenyewe?

Siyo kwa makadirio yetu wenyewe.

Tuaweza kuamini tu juu ya kujifikiria.

Tunadhihirishwa pale tu Bwana anapoagiza. 2 Kor. 10:18, "*Maana mtu mwenye kukubaliwa si yeye ajisifuye, bali yeye asifiwaye na Bwana.*"

Hivyo basi hata kama "tutafikiria" kwamba tuko sahihi, hatuwezi kuwa waamzi wa mwisho. 1 Kor. 4:4, "*Maana sijui sababu ya kujishitaki nafsi yangu, lakini sihesabiwi haki kwa ajili hiyo; ila anihumuye mimi ni Bwana.*"

Tunaweza kukosea katika kudhani, ambayo itapelekea katika hatima mbaya kuhusu sisi wenyewe.

Paulo alifikiria kuwatesa Wakristo ilikuwa inampendeza Mungu. Mdo. 26:9-11, "*Kweli mimi mwenyewe naliona ndani ya nafsi yangu kwamba yanipasa kutenda mambo mengi yaliyopingamana na jina lake Yesu Mnazareti; nami nikayafanya hayo Yerusalemu, niliwafunga wengi miongoni mwa watakatifu ndani ya magereza nikiisha kupewa amri na wakuu wa makuhani na walipouawa nalitoa idhini yangu. Na mara nyingi katika masinagogi yote naliwaadhibu, nikawashurutisha kukufuru;*

nikawaonea hasira kama mwenyewe wazimu, nikawaudhi hata katika miji ya ugenini."

Kutakuwa na watu wengi siku ya hukumu ambao hudhani walimpendeza Mungu kipindi cha maisha yao. Mat. 7:21-23, "*Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliyembinguni. Wengi wataniambia siku ile Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu ninyi mtendao maovu.*"

Hivyo tunapaswa kuangalia viwango vya nje yetu binafsi ambayo tunajichunguza!

Sio kwa makadirio ya watu wengine.

Hatuwezi kujilinganisha na wengine, au kuamini udhibitisho wao.

Siyo vyema tujilinganishe na wengine. 2 Kor. 10:12, "*Kwa kuwa hatudhubutu kujihesabu pamoja na baadhi yao wanaojisifu wenyewe wala kujilinganisha nao; bali wao wenyewe wakijipima nafsi zao na nafsi zao, hawana akili.*"

Uthibitisho wa wengine ni kitu kidogo. 1 Kor. 4:3, "*Lakini kwangu mimi si kitu kabisa nihukumiwe na ninyi, wala kwa hukumu ya kibinadamu, wala sijihukumu hata nafsi yangu.*"

Mara nyingi watu hukosea katika mawazo yao na makadirio.

Wengi watajikuta wamepotea siku ya hukumu. Mat. 7:13-14, "*Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba, maana mlango ni mpana na njia ni pana iendayo upotevuni nao ni wengi waingiao kwa mlango huo, bali mlango ni mwembamba na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache.*"

Hata dini nyingi zitashangazwa. Mat. 7:21-23, "*Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliyembinguni. Wengi wataniambia siku ile Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu ninyi mtendao maovu.*"

Lazima tutafute kiwango kingine ambacho tutaweza kujichunguza wenyewe.

Lazima tujijaribu wenyewe kwa kiwango cha neno la Mungu.

Tena, ni ushauri wa Bwana ndo unaomfanya mtu athibitishwe. 2 Kor. 10:18, "*Maana mtu mwenye kukubaliwa si yeye asifuye, bali yeye asifiwaye na Bwana.*"

Bwana ndiye mwamzi wa mwisho.

- 1 Kor. 4:4, "*Maana sijui sababu ya kujishitaki nafsi yangu, lakini sihesabiwi haki kwa ajili hiyo; ila anihumuye mimi ni Bwana.*"
- 2 Kor. 5:10, "*Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya.*"

Kama Bwana mwenyewe alivyosema, tutahukumiwa kwa neno lake. Yohana 12:48, "*Yeye anikataaye mimi, asiyekubali maneno yangu anaye amhukumuye; neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho.*"

Kiwango pekee ambacho ni sahihi cha kutumia tunapojichunguza ni neno la Mungu. Hatupaswi kuamini hisia zetu, au ambacho wanakisema wengine.

Mwisho, ngoja nishiriki nanyi baadhi ya haya…

Maswali ambayo yatatusaidia kujichunguza wenyewe ni je Kristo kweli yu ndani yangu?

Je nimemvaa katika ubatizo? Gal. 3:27, "*Maana ninyi nyote mlibatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.*"

Je nazitunza maagizo yake?

Yohana14:21, "*Yeye aliye na amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.*"

Je "alama" za utume zinakuja katika maisha yangu?

Je nakaa katika neno lake? Yohana 8:31, "*Basi Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli.*"

Je nazaa matunda? Yohana 15:8, "*Hivyo hutukuzwa Baba yangu, kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi wangu.*"

Kama matunda ya Roho. Gal. 5:22-23, "*Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria.*"

Kama matunda ya midomo yetu tunapomsifu Mungu. Heb. 13:15, "*Basi kwa njia yake yeye, na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani tunda la midomo iliungamayo jina lake.*"

Kama matunda ya kazi njema.

- Tit. 2:14, "*Ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema.*"
- Tit.3:8, "*Ni neno la kuaminiwa na mambo hayo nataka uyanene kwa nguvu ili wale waliomwamini Mungu wakumbuke kuhudumu katika matendo mema. Hayo ni mazuri tena yanafaida kwa wanadamu.*"
- Tit. 3:14, "*Watu wetu nao wajifunze kudumu katika matendo mema, kwa matumizi yaliyo lazima ili wasiwe hawana matunda.*"

Je nina tabia za wale waliokuwa wanafunzi wa kweli?

Chini ya uvuvio, Paulo aliandika 2 Kor.13:6, "*Lakini natumaini kama mtajua ya kuwa sisi hatukukataliwa.*"

Tunaweza kuwa na mawazo ya mtume wa kweli kutoka: Fil. 3:7-14, "*Lakini mambo yale yaliyokuwa faida kwangu naliyahesabu kuwa hasara kwa ajili ya Kristo. Naam, zaidi ya hayo nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu, ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nipate Kristo; tena nionekane katika yeye, nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu kwa imani; ili nimjue*

yeye na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake nikifananishwa na kufa kwake; ili nipate kwa njia yoyote kuifikia kiama ya wafu. Si kwamba nimekwisha kufika, au nimekwisha kuwa mkamilifu; la! Bali nakaza mwendo ili nipate kushika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu. Ndugu sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu."

- Tunasoma kuhusu lengo lake katika maisha (7-11).
- Tunasoma kuhusu nia yake katika kutimiza lengo hilo (12-14).

WOTE tutakuwa na "fremu ya akili" kama tukiwa "katika imani" na "Kristo ndani yetu". Fil. 3:15-17, "*Basi sisi tulio wakamilifu na tuwaze hayo na hata mkiwaza mengine katika jambo lolote, Mungu atawafunulia hilo nalo. Lakini hapo tulipofika na tuenende katika lilo hilo. Ndugu zangu mnifuate mimi, mkawatazame wao waendao kwa kuufuata mfaano tuliowapa ninyi.*"

Hitimisho

Maswali mengine yatakuwa sahihi kuuliza tunapojihoji wenyewe, lakini nadhani maelezo haya yanaonyesha jinsi tunavyopaswa kutumia neno la Mungu "kujithibitisha" wenyewe.

Fikiriaa hali ya hao "walioachwa", "wasio na sifa" "walioshindwa jaribio".

Paulo anaelezea baadhi yao katika: Fil. 3:18-19, "*Maana wengi huenenda ambao nimewaambieni mara nyingi habari zao, na sasa nawaambia hata kwa machozi , kuwa ni adui za msalaba wa Kristo; mwisho wao ni uharibifu, mungu wao ni tumbo, utukufu wao u katika fedheha yao, waniao mambo ya duniani.*"

Kwa sababu wameweka akili yao kwenye mambo ya dunia, mwisho wao ni uharibifu!

Ni bora kiasi gani kuwa kama wale walio elezewa katika Fil. 3:20-21, "*Kwa maana sisi wenyeji wetu uko mbinguni; kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi Bwana Yesu Kristo; atakayeubadili mwili wetu wa unyonge upate kufanana na mwili wake wa utukufu,*

kwa uwezo ule ambao kwa huo aweza hata kuvitiisha vitu vyote viwe chini yake."

Kuhakikisha kwamba "*hutaachwa*", hivyo mara zote "*jichunguzenu wenyewe*" katika nuru ya neno la Mungu!

Kujichunguza wenyewe tunaposhiriki ushirika wa meza ya Bwana ni aina tofauti ya kujichunguza. 1 Kor. 11:23-29, "*Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate, naye akiisha kushukuru akaumega, akasema huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanye hivi kwa ukumbusho wangu. Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu. Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo. Basi kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho chaa Bwana isivyostahili, atakuwa amajipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana. lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate na kukinywea kikombe. Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili.*"

Uchunguzi tunaotakiwa kufanya hapa ni kuchunguza kama tunafikiria kuhusu dhabihu ambayo Kristo alifanya kwa ajili yetu tunaposhiriki meza ya Bwana. Kama tunafikiri kuhusu kitu kingine, hatuufikiri mwili wa Kristo na tuna hatia ya mwili na damu yake.

Hili ni jambo muhimu naa hatupaswi kulichukulia kirahisi.